Riport ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Kitaifa Mkoani Kagera Mwaka 2011.

Awali ya yote tuna mshukuru Mungu kwa kutuwezesha kusafiri salama katika safari ya kwenda na kurudi. Pia tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa baraza la taifa la usalama barabarani kwa kutuwezesha kiuchumi na kuweza kushiriki maazimisho hayo. Shukrani tena jeshi la polisi kikosi cha usalama barabarani makao makuu Dar es Salaam chini ya usimamizi wa kamanda mkuu wa kikosi cha usalama barabarani Tanzania, Mh Mohamedi Mpinga ambaye pia ni k/tibu mkuu wa baraza la taifa la usalama barabarani tanzania. Shukrani kwa walezi wetu wa UWABA Inspector Abeli Swai na Sara Bundara, kwa ushirikiano wao mkubwa sana kama walezi wetu kwa kuhakikisha UWABA tuna shiriki ma azimisho hayo, mwisho shukrani kwa uongozi wa uwaba na wanachama wote kwa maombi na baraka zenu juu ya safari yetu.

Wafuatao ndio tulio wakilisha UWABA katika maazimisho hayo; Filbert Mbecha, Dominatha Rwechungura, Hussen H. Hamisi na Hamadi H. Bwaja.

Tuliondoka tar 29/09/2011 hadi kahama[saa tatu jioni] na kufika Bukoba siku ya pili tar 30/09/2011[saa sita mchana] tulimjulisha RTO wa Kagera kuwa tumewasili na alitukaribisha ofisini kwake. Na baada ya kulipoti kwake. Tuli lipoti kwake tena ofisini kwake siku ya pili na kumpa mpango kazi wetu wa kufundisha . Baada ya hapo tulitembelea viwanja vya maonyesho vijulikanavyo kama jimukana, kuangalia uwezekano wa kupata nafasi ya sisi kutoa elimu. Tuliweza kuonana na kamanda Mpinga na kumueleza kuhusu hilo alisema atafanya utaratibu wa kuhakikisha tunakuwa pamoja katika banda moja na jeshi la polisi na ilikuwa hivyo.

tar 3/10/2011 Maazimisho yalianza rasmi na; yalianza kwa maandamano tokea stendi kuu ya Bukoba mjini hadi viwanja vya jimukana, yaki ongozwa na watembea kwa miguu, gari la matangazo, wapanda baiskeli , wapanda pikipiki, mikokoteni na mwisho magari nyimbo nderemo na vifijo vikichombezwa na kupokelewa na mgeni rasmi Mh Jaji Mkuu Mohamed Chande Othman.

Baada ya maandamano kupokelewa na kusikia hotuba, elimu ilianza kutolewa ktk ma banda. Tar 4/10/2011 Hamadi Bwaja aliambatana na traffic kwenda kufundisha s/msingi Rumuli na Hussen Hamza alienda kufundisha a/msingi Kibeta na Kitendaguro. Filbert alibaki katika banda na kutoa elimu akisaidiana na Rwechungura ambaye alivutiwa sana kufanya kazi ya mc.

tar 5/10/2011 baraza la taifa la usalama barabarani na wadau walitembelea baadhi ya maeneo ambayo nihatari sana kwa ajali katika njia za mkoani Kagera ukielekea Uganda na kuweza kupata mchango wa mawazo wa namna ya kuweza kuepusha ajali hizo kuendelea kutokea. Kwa upande wetu Hamadi Bwaja aliwakilisha.

tar 7/10/2011 Filbert , Hamadi , na Hussen tulienda kufundisha wanafunzi hamsini wa s/msingi Rumuli kwa nadharia na vitendo ambao walipewa miongozo, kujaza evaluation kama wame elewa mafunzo, vipi wataweza kubadilika na baada ya mafunzo hayo tulimpa vyeti mlezi wetu Afande Swai ili avisaini.

Tar8/10/2011 ilikuwa ni kilele cha maazimisho na yalifungwa kwa mandamano tena kama ilivyo kuwa siku ya ufunguzi na kupokelewa na Mkuu wa Mkoa wa Kagera Mh Fabian Massawe. Zawadi mbali mbali zilitolewa kwa s/za msingi zilizo shindaniwa nyimbo, maigizo na ngonjera. Sambamba na vyeti kwa wanafunzi walio fuzu mafunzo ya elimu ya nadharia na vitendo ya usalama barabarani kwa wapanda baiskeli, ambao wanafunzi wa tano wa s/msingi Rumuli walikabidhiwa vyeti na Mgeni Rasmi aliyefunga maazimisho hayo ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Kagera wakiwa wakilisha wenzao hamsini.

Katika muda wasiku zote za ma azimisho tumefundisha jumla ya wanafunzi 450 ambao kati ya hao wanafunzi 100 kutoka shule ya msingi ya Tumaini na 350 kutoka shule ya msingi Rumuli. Pia tulifanikiwa kutembelewa na washiriki 239 ambao nao walipata elimu kupitia bandani ambao waliweza pia kusaini katika kitabu chetu cha wageni tulicho kuwa tumeweka mezani.

Kati yao pia tuliweza kupata jumla ya ma RTO sita [6] kutoka mkoni Tanga, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Kilimanjaro na Kigoma nao pia walipata fursa ya kufika ktk banda letu na kuwapa elimu. Kwahiyo jumla tume toa elimu ya usalama barabarani kwa wapanda baiskeli 639 kwa muda wote wa wiki la maazimisho hayo.

<u>Changamoto</u>; tumepata changamoto nyingi sana zikiwemo , mahitaji ya miongozo ya kufundishia , reflector jacket, helmet, kwa wadau wengi ambao walikuwa wanakiu ya kupewa ilikujifunza zaidi kwa kile walicho fundishwa. Pia wadau wengi ambao walifanikiwa kuja kupata elimu wali sisitiza huduma tunayo toa iwafikie na wapanda baiskeli wengine mikoani.

<u>Matatizo</u>; kuna mwanafunzi mmoja wa s/ msingi Rumuli aliibiwa baiskeli yake katika viwanja vya maonyesho baada ya kuipaki na yeye kwenda kuangalia michezo iliyokuwa inaendeshwa uwanjani hapo. Pia kuna mwanafunzi aitwaye Emanuel Senforian wa s/msingi Rumuli aliye anguka na baiskeli na kupata mchubuko ktk goti wakati tumekabiziwa na mwalimu wao wa michezo, Hussen Hamza alimkibiza hospitali ya mkoa na kwa matibabu kwa gharama zetu UWABA.

<u>Maboresho</u>; yafuatayo tumeyaona ni vyema tuka boresha mwongozo wa kufundishia kwa kuuprint kwa rangi, vyeti pia viwe vya rangi, tuwe na maandalizi ya kuandaa mchanganuo[proposal] mwanzoni mwa mwaka ilikujiandaa vyema ilikushiriki pasipo maandalizi ya kutosha. Muhimu tuwe na kamera ya chama ilikuchukua kumbukumbu ya matukio, badala ya kuazima kila mwaka, pia tuwe na vijarida ambavyo vita kuwa na maelezo ya kuitambulisha uwaba ikelezea kazi zake ,malengo yake na mafanikio. Mwisho tuwe na hema.

<u>Mafanikio;</u> tumepata cheti cha ushiriki wetu kama moja ya wadau wa kutoa elimu ya usalama barabarani kwa wapanda baiskeli, kutoka balaza la taifa la usalama barabarani Tanzania.

Mwisho wa riport.na imeandikwa na Filbert Mbecha, kwa ushirikiano wa timu nzima iliyo shiriki maazimisho hayo.

…….